JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA TANO

23 JUNI, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA TANO – TAREHE 23 JUNI, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

655. MHESHIMIWA JOHN JOHN NCHIMBI (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya Wataalam wa Kigeni wanaokaa muda mchache na kupatiwa *Business Visa* ambayo haitambuliwi na Idara ya Kazi.

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

656. MHESHIMIWA CLAYTON REVOCATUS CHIPANDO (KIGOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha za Mfuko wa Barabara ili kuboresha Barabara za ndani ya Manispaa ya Kigoma Ujiji.

657. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (TEMEKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Azimio - Mashine ya Maji - kwa Mama Kibonge mpaka Buza Sheli.

658. MHESHIMIWA DKT. YAHAYA ESMAIL NAWANDA (NEWALA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, nini mpango wa Serikali kuongeza magari ya kutoa huduma katika Halmashauri ya Wilaya Newala.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

659. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, lini Mfumo wa Kidijitali wa *One-Stop Centre* utakaounganisha Taasisi kama TIC, BRELA na TRA utakamilika ili kuboresha biashara na uwekezaji.

WIZARA YA UCHUKUZI:

660. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, mbali na usafiri wa Ndege na SGR, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha usafiri wa Umma unazingatia mahitaji ya Watu wenye Ulemavu.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

661. MHESHIMIWA YAGI MAULID KIARATU (SINGIDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo Kikuu katika Mkoa wa Singida ili kuongeza fursa za Elimu ya Juu kwa Vijana wa eneo hilo.

WIZARA YA UJENZI:

662. MHESHIMIWA EDWARD KISAU OLELEKAITA (KITETO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Kongwa – Kiteto – Simanjiro – Arusha utaanza kwa kiwango cha lami.

663. MHESHIMIWA MECKTRIDIS FRATERN MDAKU (MALINYI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa Kivuko cha Kikove kinachounganisha Wilaya ya Malinyi na Jimbo la Mlimba.

WIZARA YA MAJI:

664. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa Maji wa Vijiji 8 katika Wilaya ya Siha utakamilika.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

665. MHESHIMIWA THOMAS MGONTO KITIMA (IKUNGI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha Kongani za Viwanda katika Jimbo la Ikungi Mashariki.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

666. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka masharti kwa Wafanyabiashara wanaovuna miti ili wachangie kwenye upandaji wa miti au Mfuko wa TFS.

WIZARA YA KILIMO:

667. MHESHIMIWA ENOCK ZADOCK KOOLA (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Zao la Kahawa ili kurejesha heshima ya Mkoa wa Kilimanjaro.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

(Majadiliano yanaendelea)

IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa kwa Hatua zake zote)

Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi wa Mwaka 2026 *(The Appropriation Bill, 2026)*.

DODOMA
23 JUNI, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE